RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

BIASHARA YA UFUGAJI BORA WA KUKU WA ASILI

KITABU CHA MWONGOZO

inter cooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

swisscontact

RLDC na Uboreshaji wa Maisha Vijijini

Shirika la Rural Livelihood Development Company (RLDC ni moja ya mafanikio ya ushirikaiano kati ya Tanzania na Uswisi kwenye mchakato wa kupambana na umaskini na kuboresha maisha ya jamii za vijijini. Hii ni taasisi isiyo ya kibiashara ili yoanzishwa mwaka 2005 na mashirika ya Intercooperation na Swisscontact, lengo kuu likiwa kutekeleza Programu ya kuendeleza maisha ya jamii za vijijini (RLDP). Programu hii inasha bihiana na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupambana na Umaskini (MKUKUTA). Dhamira kuu ya RLDC ni Kuendeleza/kuboresha mifu mo ya masoko ili kuwawezesha wazalishaji wa vijijini kutumia
fursa zilipo kuboresha maisha yao.

Kwa sasa, RLDC inatelekeleza awamu ya pili ya mpango wake (2008-2011) na inaweka msukumo zaidi kwenye uendelezaji wa mifumo ya masoko. RLDC inafanya kazi katika mikoa sita ya Kanda ya kati-Dodoma, Singida, Morogoro, Shinyanga, Tabora, na Manyara. Jamii nyingi maskini zinaishi katika ukanda huu wenye sehemu kubwa yenye hali ya mvua chache na nusu jangwa inayostawisha shughuli chache za kiuchumi.

Hata hivyo kuna fursa nyingi sana zinazoweza kutoa ajira na kuboresha ya jamii zake. RLDC inafadhiliwa na Serikali ya Uswisi kupitia shirika la Uswisi la maendeleo (SDC).

Kwa sasa RLDC inawezesha sekta za pamba, alizeti, maziwa, ufugaji wa kuku wa kienyeji, mpunga na habari kupitia vipindi vya redio kwa ajili ya wazalishaji wa vijijini.

“RLDC inaboresha mifumo ya masoko ili kuwezesha wazalishaji wa vijijini kuinua maisha yao”

RURAL LIVELIHOOD DEVELOPMENT COMPANY

BIASHARA YA UFUGAJI BORA WA KUKU WA ASILI

MWONGOZO

inter cooperation

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederazium svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

swisscontact

YALIYOMO

Utangulizi **1**

Sehemu ya Kwanza **2**
Njia tofauti za kufuga kuku

Sehemu ya Pili **5**
Banda la Kuku: Sifa za banda bora la Kuku

Sehemu ya Tatu **9**
Kuzaliana na kutotolesha : Uchaguzi wa Kuku bora

Sehemu ya Nne **13**
Utunzaji wa Kuku

Sehemu ya Tano **16**
Magonjwa ya Kuku

Sehemu ya Sita **19**
Kusimamia Ufugaji Wako: Kutunza kumbukumbu

Sehemu ya Saba **22**
Masoko

Sehemu ya Nane **24**
Chama cha Akiba na Kukopa

Utangulizi

Tanzania ina idadi ya kuku wa kienyeji wanaokadiriwa kuwa million 34 ambao wanafugwa kwa mtindo wa huria. Ufugaji wa aina hii hufanyika vijijini na mijini pia.

Idadi hii ya kuku bado ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Watanzania wanaokadiriwa kuwa milioni 40 (sensa ya mwakaxxx). Ulaji wa nyama ya kuku nchini unakadiriwa kuwa ni wastani wa kilo 0.7 kwa kila mtu kwa mwaka mzima ilihali Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) linakadiria wastani mzuri wa ulaji wa nyama kuwa ni kilo 6.8 kwa mtu kwa mwaka. Hii inaashiria kuwa soko la kuku nchini ni kubwa, ambayo ni fursa muhimu kwa wafugaji wa kuku.

Ufugaji wa kuku ni nyenzo nzuri ya kujipatia kipato katika kaya kwa sababu ufugaji wa kuku hauhitaji mtaji mkubwa na hauna kazi kubwa kiuendeshaji. Katika ufugaji huria kuku hujitafutia chakula wenyewe. Pia inapowezekana hupewa mabaki ya chakula, chenga, pumba au nafaka yoyote inayopatikana katika mazingira husika. Kwa walio wengi ifikapo nyakati za jioni, kuku hulala jikoni au ndani nyumbani kwa mfugaji mwenyewe. Ufugaji huu ni rahisi kwa kuwa hauna gharama kubwa ila faida yake ni kitoweo tu au fedha kidogo sana.

Kutokana na lishe duni na kuzaana wenyewe kwa wenyewe (bila kubadili jogoo), kuku wa kienyeji walio wengi wana uzito mdogo. Wana wastani wa uzito wa robo tatu za kilo hadi kilo moja wakiwa na umri wa zaidi ya mwaka mmoja. Ila wakitunzwa vizuri zaidi na kuboreshwa wana uwezo wa kufikia uzito wa kilo moja hadi moja na nusu katika umri wa miezi sita hadi nane.

Kwa upande wa utagaji wa mayai kuku wa kienyeji kwa wastani hutaga mayai 50 hadi 65 kwa mwaka. Wakitunzwa vizuri zaidi huweza kufikia uzalishaji wa mayai 80 hadi 100 kwa mwaka.

Kijitabu hiki kinatoa maelezo ya njia na kanuni mbalimbali rahisi za kuzingatia ili mfugaji aweze kuzitumia kupata mazao mengi na bora zaidi yatakayomnufaisha kimapato na kwa matumizi mengine. Kanuni hizi ni pamoja na:

- √ Kuchagua njia bora ya kufuga na sifa za mabanda bora ya kuku
- √ Kuchagua aina bora ya kuku wa kufuga, kuzaliana na kutotolesha
- √ Utunzaji wa vifaranga
- √ Kutengeneza chakula bora cha kuku
- √ Kudhibiti na kutibu magonjwa
- √ Kutunza kumbukumbu
- √ Kutafuta masoko

Sehemu ya Kwanza

Njia tofauti za kufuga kuku

Mambo yanayomfanya mfugaji kuamua atumie njia fulani ya kufuga ni pamoja na uwezo wa kugharamia shughuli ya ufugaji wa kuku na ukubwa wa eneo alilonalo la kufugia. Katika sehemu hii utajifunza njia tatu za kufuga kuku ambazo ni:

1. Kufuga huria

Kuku huachwa wenyewe kujitafutia chakula na maji. Njia hii inatumika zaidi kufuga kuku wa kienyeji. Mara chache sana mfugaji huwapatia kuku chakula cha ziada. Kwa ufugaji huu lazima kuwe na eneo kubwa la kutosha kuku kuzunguka na kutafuta chakula. Kuku hulala eneo lisilo rasmi kama vile jikoni, kwenye kiambata n.k.

Ufugaji huria

Faida zake

- Ni njia rahisi ya kufuga.
- Gharama yake pia ni ndogo.
- Kuku wanapata mazoezi ya kutosha.
- Kuku wanapata chakula mchanganyiko ambacho kinafaa kiafya.

Hasara zake

- Kuku huwa hatarini kuibiwa au kudhurika na wanyama wakali na hali mbaya ya hewa.
- Ukuaji wa kuku ni hafifu, hufikia uzito wa kilo 1.2 baada ya mwaka.
- Huharibu mazingira kama kula na mimea ya bustanini mazao kama nafaka.
- Ni rahisi kuambukizwa magonjwa.

2. Kufuga nusu ndani – nusu nje

Huu ni mtindo wa kufuga ambapo kuku wanakuwa na banda lililounganishwana uzio kwa upande wa mbele. Hapa kuku wanaweza kushinda ndani ya banda au nje ya banda wakiwa ndani ya uzio.

Ufugaji wa nusu ndani na nusu nje

Wakati wa mchana kuku huwa huru kushinda ndani ya banda hasa wanapotaka kutaga na wakati wa kuatamia au wanaweza kukaa ndani ya uzio nje.

Faida za kufuga nusu ndani na nusu nje

- Kuku wanakuwa salama mbali na maadui mbali mbali.
- Utaweza kuwalisha kuku wako vizuri hivyo wataweza kuongeza uzalishaji wa mayai na wa nyama (kwa kukua haraka).
- Itakuwa rahisi kwako kudhibiti wadudu na vimelea vinavyoweza kuleta magonjwa kwa kuku wako.
- Ni rahisi kuwatenganisha kuku katika makundi tofauti na kuwahudumia ipasavyo.
- Ni rahisi kutambua kuku wagonjwa kuliko kufuga huria.
- Kuku watapata mwanga wa jua wa kutosha pamoja na hewa safi.Wakati wa jua kali watakuwa huru kuingia ndani ya banda na kukaa kivulini.
- Kuku hawatafanya huharibifu wa mazao yako shambani au bustanini na kwa majirani zako.
- Utapata urahisi wa kukusanya na kupeleka mbolea bustanini au shambani.

Changamoto ya kufuga nusu ndani na nusu nje

- Huna budi uwe na muda wa kutosha kwa ajili ya kuwahudumia kuku wako.
- Pia utahitaji kuwa na eneo kubwa kiasi la kufugia.
- Pia utaingia gharama ya ziada kidogo ya kutengeneza banda na wigo na kuwapatia uku chakula cha ziada.
- Hata hivyo gharama za muda huo na za vifaa vingine zitafidiwa na mapato ya ziada utakayopata kwa kufuga kwa njia hii.

3. Kufuga ndani ya Banda tu

Njia nyingine ni kuwafuga kuku ndani tu. Katika njia hii, kuku hukaa ndani wakati wote. Njia hii ya ufugaji utumiwa zaidi na wafugaji wa kuku wa kisasa. Lakini yaweza kutumika hata kwa kuku wa asili hasa katika sehemu zenye ufinyu wa maeneo.

Changamoto za ufugaji wa ndani ya banda tu

- Unatakiwa uwe na muda wa kutosha wa kuwahudumia kuku wako kikamilifu.
- Pia unatakiwa kuwa na mtaji mkubwa wa kujenga banda na kuwanunulia kuku chakula.
- Ugonjwa ukiingia na rahisi kuambukizana.Vilevile kuku huweza kuanza tabia mbaya kama kudonoana, n.k.

Faida za kufuga ndani tu

- Ni rahisi kutambua na kudhibiti magonjwa.
- Ni rahisi kudhibiti upotevu wa kuku, mayai na vifaranga.
- Ni rahisi kuwapatia chakula kulingana na mahitaji ya kila kundi.
- Ni rahisi kuwatambua na kuwaondoa kuku wasiozalisha katika kundi.

Ni ufugaji upi unafaa zaidi kutumika kwenye mazingira ya vijijini?

Kwa ujumla, njia rahisi na inayopendekezwa kutumiwa na mfugaji wa kawaida kijijini ni ya ufugaji wa nusu ndani na nusu nje, yaani nusu huria. Hii inatokana na faida zake kama zilizoainishwa hapo awali. Kwa kutumia mfumo huu wa ufugaji, utaepuka hasara za kufuga kwa mtindo wa huria kama zilivyainishwa mwanzoni mwa sehemu hii ya kitabu hiki.

Pia ukitumia mtindo wa ufugaji wa nusu huria utafanya ufugaji wako kwa njia bora zaidi ndani ya uwezo ulionao, kwa sababu kwa sehemu kubwa utatumia mali ghafi inayopatikana katika eneo lako.

Sehemu ya Pili

Banda la Kuku

Sifa za banda bora la Kuku

Ukiamua kufuga katika banda kwa njia mbili zilizoelezwa awali utatakiwa kujenga banda lenye sifa zitakazokidhi mahitaji ya msingi ya kuku. Banda bora la kuku linatakiwa kuwa kama ifuatavyo:

Liwe jengo imara

- Pasiwe na sehemu zilizo wazi kwenye msingi na kati ya ukuta na paa.
- Banda lijengwe na vifaa vinavyopatikana katika mazingira yako ili liwe na gharama utakayoweza kumudu.
- Unaweza kutumia matofali ya udongo, udongo, miti, fito,n.k. Ukitumia fito au mabanzi ondoa maganda ili kuthibiti mchwa.
- Jengo mara litazuia maadui kama panya, vicheche, paka, nyoka na wezi kuingia ndani ya banda na kuwadhuru au kuwaiba kuku.

Liwe rahisi kusafisha

- Kuta na sakafu visiribwe zisiwe na nyufa ili kurahisisha kusafisha.
- Pia itadhibiti kusiwe na wadudu wa kujificha katika nyufa kama papasi, viroboto n.k.
- Sakafu ya banda lazima iwekewe matandazo kama pumba ya mpunga au maranda ya mbao au mabaki ya mazao au nyasi kavu kutegemeana na kinachopatikana kwa urahisi katika mazingira yako.
- Matandazo haya husaidia kunyonya unyevu unaotokana na kinyesi cha kuku au maji yanayomwagika katika banda.
- Banda hubakia kavu bila kuwa na harufu mbaya na wadudu kama inzi hata vimelea vya magonjwa hudhibitiwa.

Eneo la nje kuzunguka banda kuwe na usafi wa kudumu

Hali ya usafi nje ya banda itafanya wadudu kama siafu au mchwa na wanyama kama panya na paka mwitu wakose maficho. Nje ya banda ndani ya uzio kuwe na miti midogo na mimea mingine midogo kwa ajili ya kivuli.

Ufugaji nusu huria

Liwe na nafasi ya kutosha kwa kuku waliopo: Kwa kawaida eneo la mita mraba moja hutosha kuku wanne wanaotaga au kuku 8 wa nyama. Nafasi ya mita mraba 1 inatosha vifaranga 16 hadi kufikia umri wa majuma manne.

Ufugaji wa nusu huria

Liweze kuingiza hewa na mwanga wa kutosha: Banda linaloweza kuingiza hewa safi na kutoka ndani yake hubaki kavu. Harufu mbaya hutoka na kuku huweza kupumua hewa safi. Hii husaidia pia kudhibiti kuzaliana kwa vimelea vinavyosababisha magonjwa,hivyo hudhibiti magonjwa.

Lisiwe na joto sana au baridi sana: Panda miti ya kuzunguka banda lako ili eneo liwe na kivuli cha kutosha na pia lisiwe na upepo mkali.Kama hali halisi ya eneo la kufugia ina joto kubwa kwa vipindi virefu paa la banda wakati wa ujenzi liinuliwe juu zaidi kuruhusu mzunguko zaidi wa hewa na joto la paa (kama ni la bati) liwe mbali juu ya kuku.

Joto kwenye banda linaweza kusababishwa na msongamano wa kuku, hivyo mfugaji aangalie aweke idadi ya kuku inayowiana na ukubwa wa banda lake.

Paa

Liwe imara na lisilovuja. Waweza kutumia mabati, nyasi, madebe, makuti n.k. kutegemeana na upatikanaji wa vifaa vya kuezekea.Wakati wa kuezeka paa lisiishie karibu sana na ukuta bali liwe na sehemu kubwa iliyozidi ukuta kuzuia mvua kuingia ndani kama ni ya upepo (angalia mchoro hapa chini).



Paa lifunike ukuta kwa sehemu kubwa

Vifaa vinavyohitajika katika banda la kuku

Kuku wakifugwa kwa mtindo wa nusu ndani na nusu nje wanahitaji huduma mbalimbali ndani ya banda na ndani ya wigo. Ili kutoa huduma hizi vifaa vifuatavyo ni muhimu viwe katika banda:

Vyombo vya Maji

Kuna njia nyingi za kutengeneza vyombo vya kuwekea maji ya kuku ya kunywa.



Kinywesheo cha kujitengenezea

Kinywesheo

- Aina ya mojawapo unayoweza kutumia ndoo au debe la lita kumi au ishirini ya plastiki. Kata ndoo hiyo pande nne kutoa nafasi ya kuku ya kunywea kama kielelezo kinavyoonyesha. Tengeneza idadi ya vyombo hivi inayowiana na wingi wa kuku ulionao.
- Au waweza kutumia sufuria au beseni pana kiasi. Hii huwekewa tofali au jiwe safi pana baada ya kuwekewa maji ya kunywa ili kuzuia kuku wadogo wasizame na maji yasichafiliwe kirahisi.
- Vifaa maalum vya kunyweshea kuku vinapatikana katika maduka ya pembejeo za kilimo.

Vyombo vya Chakula

Vyombo hivi ni muhimu viwe vimetengenezwa vizuri ili visiwe chanzo cha upoteaji wa chakula. Unapotengeneza kilishio cha kuku kumbuka kuwa kuku wana tabia ya kuchakura. Husambaza au kupekua chakula kwa miguu hata kwa midomo ili kupata chakula cha chini.



Kilishio

Tabia hii husababisha kumwagwa kwa chakula kingi chini na kusababisha hasara. Unaweza kudhibiti tatizo hili kwa kutengeneza vyombo visivyoruhusu kuku kuchakura kama inavyoonyeshwa kwenye kielelezo hapa chini.

Unaweza kutengeneza kilishio hiki wewe mwenyewe au fundi seremala waliopo katika eneo unaloishi. Inafaa kilishio kiwe chembamba ili kuku wasiweze kuingia. Pia kinatakiwa kiwe kirefu ili kuku waweze kula bila kusongamana.

Viota

Zipo aina tofauti za viota ambazo hutumika kwa ajili ya kutagia. Ipo aina ya ambayo ni ya kutagia kuku mmoja mmoja. Vipimo vinavyopendekezwa kwa kila kiota ni upana wa sentimita 30, urefu sentimita 30 na kina sentimita 35. Upande wa mbele uachwe wazi

ila sentimita 10 za kwanza kutoka chini zizibwe na ubao (angalia kielelezo). Weka idadi ya viota inayotosheleza kuku ulio nao.

Muunganiko wa Viota

Pia ipo aina nyingine inayoweza kutumiwa na kuku zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja. Ni kama kiota kimoja kilichogawanywa katika vyumba kadhaa. Ila kila chumba kina vipimo kama vya kiota kimoja(angalia picha hapa chini).Aina hii ya kiota ina upana wa sentimita 30 na kina sentimeta 35 na urefu wake unategemea idadi ya viota.

Viota vinatakiwa kuwa na giza ili kuku wasiogope kuingia kutaga ndani yake. Pia giza husaidia kupunguza tabia ya kuku kula mayai na kudonoana. Kiota kinafaa kuwekwa mahali ambako ni rahisi kuku kuingia na kutoka. Vile vile iwe ni sehemu itakayorahisisha usafishaji wa kiota chenyewe.

Vichanja

Kuku wana asili ya kupenda kulala au kupumzika sehemu iliyoinuka. Hivyo ndani ya banda weka vichanja vitakavyotosheleza idadi ya kuku waliopo.

Vichanja

Sehemu ya Tatu

Kuzaliana na kutotolesha

Uchaguzi wa Kuku bora

Ili upate kundi lenye kuku bora huna budi uchague jogoo bora na matetea bora wa kuzalisha kundi lako.

Angalia sifa zifuatazo unapochagua:

- Tetea na jogoo wawe na umbo kubwa.
- Wanaokua haraka.
- Wenye uwezo wa kustahimili magonjwa.
- Matetea wanaoweza kutaga mayai mengi.
- Matetea wanaweza kuatamia na hatimaye kutotoa vifarangakwa wingi na kuvilea.
- Jogoo unaowachagua kwa ajili ya matetea au makoo yako wasiwe na uhusiano wa damu.

Ukiishachagua wazazi wa kundi lako changanya jogoo na matetea kwa uwiano wa jogoo mmoja kwa matetea 10 hadi 12. Ukiwa na matetea 20 utahitaji kuwa na jogoo wawili.

- Nchini kwetu zipo aina tofauti za kuku wa asili ambao wana sifa tofauti. Wafugaji wengi hufuga kutegemeana na uwezo wa kuku kuhimili magonjwa ,kuwa na uzito mkubwa, utagaji wa mayai mengi n.k. Koo za kuku wa asili wenye sifa za namna hii ni aina ya Bukini , Kuchi, Kuchere na wa Kawaida wasio na ukoo maalum. Hawa kwa ujumla wao wakitunzwa vizuri wana uwezo wa kufanya vyema katika mazingira ya ya nchi hii kwa sababu wameishayazoea.

Kuatamia na kuangua mayai:

Baada ya jogoo kupanda matetea au makoo, hawa watataga mayai. Mayai yanaweza kutotoleshwa kwa njia ya asili au kwa kutumia vifaa vya kutotolesha.
Kutotoa kwa njia ya asili

Hii inafanyika kwa kuku kuatamia mayai kwa hatua zifuatazo.

Kuandaa kiota:

- Kiota kiandaliwe kabla kuku hajaanza kutaga kwa kukiwekea nyasi kavu na kuzisambaza kwa kutengeneza muundo wa kata au sahani iliyozama kidogo.
- Kiota kinyunyiziwe dawa ya unga kuua wadudu kabla na baada ya kuweka nyasi. Iwapo kuku atajiandalia kiota chake mahali panapofaa aachwe hapo ila kiota kiwekewe dawa ya kudhibiti wadudu.

Maandalizi ya kuku anayetaka kuatamia

Ufugaji wa nusu huria

Dalili za kuku anayetaka kuatamia ni:

- Anatoa sauti ya kuatamia.
- Ushungi wake umesinyaa.
- Hapendi kuondoka kwenye kiota.
- Hupenda kujikusanyia mayai mengi

Kuku wenye dalili za kutaka kuanza kuatamia akaguliwe ili kuhakikisha kuwa hawana wadudu kama utitiri, chawa, viroboto n.k. wanaoweza kumsumbua wakati wa kuatamia. Akiwa na wadudu watamsumbua hataweza kutulia kwenye kiota na kuatamia vizuri. Matokeo yake ataangua vifaranga wachache. Hivyo walio na wadudu wanyunyizie dawa ya unga kabla hawajaanza kuatamia ili kudhibiti tatizo hili.
Kuatamia

Kuku anapotaga mayai yaondolewe na kubakiza moja kwenye kiota ili kumwita kuku kuendelea kutaga. Kuku akiwa tayari kuatamia awekewe mayai kwa kuatamia. Kwa kawaida kuku mmoja anaweza kuatamia vizuri mayai 10 hadi 13 kwa wakati mmoja.

Kipindi cha kuangua mayai ni kuanzia siku 20 baada ya kuatamia. Ukitaka kutotolesha vifaranga wengi kwa wakati mmoja, kuku akianza kutaga yakusaye mayai yake na kumbakizia yai moja ili aendelee kutaga.Mayai utakayokusanya yaweke mahali pasipo na mwanga mwingi na penye ubaridi kiasi.

Fanya hivi kwa kuku kadhaa wanaotaga ndani ya muda unaokaribiana. Kila atakayeonyesha dalili ya kuanza kuatamia muwekee mayai kati ya 10 na 12 aatamie. Kwa njia hii wataatamia na kuangua ndani ya kipindi kimoja. Na utapata vifaranga wengi wa umri mmoja hatimaye kuuza kuku wengi kwa pamoja.

Kulea Vifaranga

Kulea vifaranga kwa kumtumia kuku

Baada ya vifaranga kutotolewa waache na mama yao mahali penye usalama kwa muda wa mwezi moja mbali na mwewe, vicheche, paka, kenge, n.k. Hakikisha wanapata maji na chakula cha kutosha muda wote.

Kulea vifaranga kwa kumtumia kuku

Njia nyingine ni kuwaweka vifaranga mahali pazuri na kuwafunika na tenga ili kuzuia mwewe wakati wa mchana kwa kuhakikisha kuwa hawapigwi na jua wala kunyeshewa mvua.Wakati wa usiku warejeshe kwa mama yao ili awakinge na baridi. Fanya hivi hadi wafikie umri wa mwezi mmoja ndipo uwatenge na mama yao.

Pia unaweza kutumia kifaa maalum cha kulelea vifaranga (kitalu) mara baada ya kuanguliwa. Katika kitalu wanapatiwa joto wanalohitaji. Kifaa hiki kinaweza kutengenezwakwa karatasi ngumu itumikayo kutengeza dari.(angalia mchoro unaofuata).

Au

Katika mazingira ya kijijini unaweza kutengeneza wigo wa mduara kwa magunia. Upana wake uwiane na wingi wa vifaranga ulionao na kina chake kama mita moja. Ukuta wake uwe na tabaka mbili za magunia hayo zilizoachana kwa nafasi ya inchi tatu au nne. Kati kati ya nafasi hiyo jaza maranda ya mbao au pumba za mpunga. Tayari utakuwa umepata kitalu cha kulelea vifaranga.

Kulea vifaranga kwa kumtumia kitalu

Ndani ya kitalu weka taa ya chemli ya kutoa joto linalohitajika kwa vifaranga.

Fuatilia tabia ya vifaranga wanapokuwa katika kitalu.

Wakiisogelea sana taa ina maana joto halitoshi, ongezea joto kwa kupandisha utambi. Wakienda mbali sana na taa, joto limezidi punguza. Kitalu kikiwa na joto zuri vifaranga watatawanyika kote katika kitalu na kuonyesha kuchangamka.

Mama yao akitengwa na vifaranga arudishwe kwenye kundi lenye jogoo, atapandwa na kurudia kutaga mapema. Kwa njia hii kundi la kuku litakuwa kubwa kwa muda mfupi. Kwa kawaida vifaranga wengi hufa kabla ya kufikisha miezi miwili kutokana na baridi, kuliwa na wanyama wengine na magonjwa.

Ili kudhibiti magonjwa, vifaranga wapewe chanjo dhidi ya magonjwa yafuatayo:

a. **Kideri (New castle)** siku ya 3 baada ya kuanguliwa, rudia baada ya wiki tatu kisha uchanje kila baada ya miezi mitatu.

b. **Kuhara damu au rangi ya ugoro (Coccidiosis)** : Wapewe kinga kwa dawa ya Amprolium kwa siku 3 mfululizo wanapofikisha umri wasiku 7 baada ya kuanguliwa.

c. **Gumboro** wanashusha mbawa na kujikusanya pamoja kwa baridi, pia wanaharisha nyeupe.Hutokea kuanzia wiki ya 2 hadi ya 18.Wapewe chanjo siku ya 10 hadi ya 14 baada ya kuanguliwa na rudia baada ya siku 28 na 42. Kwa magonjwa mengine angalia maelekezo sehemu ya magonjwa ndani ya mwongozo huu.

Vifaranga wapewe chakula kilichoelezwa katika sehemu ya tatu ya kijitabu hiki na maji safi ya kutosha wakati wote kwa muda wa miezi miwili. Baada ya hapo wanapewa chakula cha kuku wanaokua.

Kuku wakikaribia kupevuka wakiwa na miezi mitatu hadi minne tenganisha temba na majogoo ili kudhibiti kuku wenye uhusiano wa damu wasipandane wao kwa wao. Wakipandana na mayai yao yakianguliwa hawatatoka vifaranga wenye sifa nzuri mfano: ukuaji wao utakuwa hafifu kuliko wazazi wao, uwezo mdogo kuhimili magonjwa na wengine wanaweza kuwa na ulemavu. Pia zingatia matemba hao wasipandwe na baba yao. Vilevile majogoo hao wasimpande mama yao.

Sehemu ya Nne

Utunzaji wa Kuku

Ulishaji

Kuku kama mifugo mingine uhitaji chakula chenye virutubisho vyote vinavyohitajika mwilini ili kukua upesi na kuwa na na afya nzuri . Chakula kinachofaa ni mchanganyiko wa viini lishe mbalimbali vyenye kazi tofauti mwilini. Kila kiini lishe hakina budi kiwe katika kiwango sahihi kulingana mahitaji ya mwili wa kuku katika umri tofauti.
Kuku anahitaji chakula chenye viini lishe vifuatavyo:

Kiini lishe	**Kinapatikana katika chakula gani**	**Kazi yake mwilini**
Wanga	Pumba,Chenga za nafaka kama mahindi, mtama.	Kutia nguvu mwilini
Mafuta	Mashudu yanayopatikana baada ya kukamua mbegu za mafuta kama alizeti, karanga n.k	Kutia nguvu na joto mwilini
Protini	Mashudu ya karanga au alizeti.Damu iliyokaushwa ya wanyama kama mbuzi, ng'ombe n.k. Mbegu za jamii ya mikunde kama maharage, kunde, soya....	Kujenga mwili na kukarabati mwili
Vitamini	Majani mabichi kama mabaki ya mboga za majani, michicha ya porini, majani mabichi ya mipapai, majani ya Lusina n.k.	Kulinda mwili. Majani mabichi pia huwezesha kuku kutaga mayai yenye kiina cha njano, rangi ambayo huwavutia walaji wengi.
Madini (calsium na Fosforas)	Unga wa dagaa, unga wa mifupa iliyochomwa, chokaa	Kujenga mifupa, kutengeneza maganda ya mayai

Mfano wa kuandaa vyakula vya makundi tofauti ya kuku

Kwa Vifaranga

Kwa vifaranga vya tangu kutotolewa hadi miezi miwili tengeneza mchanganyiko ufuatao. Huu ni mfano mmojawapo wa kuandaa kilo 100 za chakula cha vifaranga. Iwapo utahitaji kuandaa jumla ya kilo 50 za chakula tumia nusu ya vipimo vilivyoainishwa katika jedwali hili.

Wastani wa mahitaji ya kuku wakubwa 50 kwa siku ni kilo 5. Chakula hiki ukigawe katika sehemu mbili na kuwapatia nusu asubuhi na nusu ya pili mchana.

Vifaranga hupewa chakula kiasi wanachoweza kumaliza (hawapimiwi).

Vifaa	**Kiasi kwa kilo**
Dagaa (unga au vichwa vya dagaa)	12 hadi 15
Chenga za nafaka kama mahindi au mtama n.k	40
Mashudu	20
Pumba	24
Chokaa	2
Unga wa Mifupa,Madini (Premix)	2
Chumvi	Robo kilo
Mchanga	1
Jumla	**Kilo 100**

Kwa kuku wanaokua (baada ya miezi miwili).

Vifaa	**Kiasi kwa kilo**
Dagaa (unga au vichwa vya dagaa)	7
Chenga za nafaka kama mahindi au mtama n.k	30
Mashudu	20
Pumba	39
Chokaa	2
Unga wa Mifupa,Madini (Premix)	2
Chumvi	Robo kilo
Mchanga	1
Jumla	**Kilo 100**

Kama umeamua kufuga kuku kwa mtindo wa kuwaacha huru wajitafutie chakula (huria) unaweza kuwapatia vifaranga nyongeza ya protini.Utafanya hivyo kwa kuwachanganyia vumbi au vichwa vya dagaa kiasi cha kikombe kimoja vilivyotwangwa pamoja na pumba ya mahindi vikombe vitano.

Maji ya Kunywa

Mfugaji ahakikishe anawapatia kuku maji masafi ya kunywa na ya kutosha kila siku. Vyombo vya maji ya kunywa budi visafishwe vizuri kila siku. Hii itasaidia sana kudhibiti magonjwa yanayoweza kutokana na vimelea vya magonjwa vinavyostawi katika maji yasiyo safi. Kuku wanaweza kuwekewa maji katika aina tofauti ya vyombo kutegemea na urahisi wa kupatikana mfano sufuria, ndoo za plastik zilizokatwa kuruhusu kuku kunywa bila kuchafua.

Usafi katika banda

Matandazo yanayowekwa katika sakafu ya banda la kuku hayana budi yageuzwe mara kwa mara kwa wastani wa kila baada ya miezi miwili au mitatu . Wakati mwingine ni kabla ya kipindi hiki muda wowote yanapoloana na maji. Matandazo uharakisha kukauka kwa unyevu katika banda unaotokana na kinyesi cha kuku na pia zaidi na maji yanayomwagika.

Usafi katika banda utasaidia kudhibiti kwa kiasi kikubwa magonjwa mbalimbali.
Kuokota mayai

Usiyaache mayai ndani ya viota kwa muda mrefu, yaokote mara kwa mara ili kuepuka kuharibiwa kwa mayai hayo na kuku wenyewe. Kuku wanayo tabia ya kula mayai yao ikiwa chakula unachowapa kina upungufu wa protini.

Vilevile kiasi cha mwanga unaoingia ndani ya banda kikizidi kuku hula mayai au kudonoana wenyewe kwa wenyewe.Uonapo dalili za namna hii kwenye kundi lako punguza kiasi cha mwanga kwa kuziba sehemu za madirisha kwa vipande vya magunia au vipande vya makasha ya karatasi ngumu.

Kama ilivyoelezwa awali kuku wapewe majani mabichi ya kutosha mara kwa mara ili wawe wanakula hayo badala ya kudonoana.

Pia fuatilia kuhakikiksha kama chakula kina protini ya kutosha. Kama tatizo la kudonoana na kula mayai litaendelea omba msaada kwa mtaalam wa mifugo akuelekeze jinsi ya kuwakata au kuwachoma midomo.

Sehemu ya Tano

Magonjwa ya Kuku

Magonjwa ya kuku yapo mengi. Hata hivyo siyo yote yanatokea mara kwa mara hapa Tanzania. Ili uweze kudhibiti yale yanayotokea katika kundi lako unahitaji kufahamu dalili za jumla za magonjwa hayo. Unapoigundua moja au zaidi ya dalili za ugonjwa au wadudu chukua hatua mara moja. Yapo magonjwa ambayo yanaweza kuangamiza kundi lote la kuku katika.muda mfupi.

Jihadhari na uwezekano wa kupatwa na hasara zinazoletwa na magonjwa ambayo unaweza kuyazuia.

Katika sehemu hii utajifunza kwa muhtasari tu dalili za jumla za magonjwa ya kuku na jinsi ya kuyadhibiti.

Dalili za Jumla za Magonjwa ya Kuku

- Kuku kupoteza hamu ya kula.
- Kuzubaa na kukaa mahali pamoja kwa muda mrefu (Kutochangamka).
- Kushuka kwa kiwango cha utagaji wa mayai.
- Vifaranga kutokua upesi au kudumaa. - Macho kuwa na rangi nyekundu.
- Kujikunja shingo.
- Kutetemeka, kutoa majimaji puani, mdomoni na machoni.
- Kutoa mharo (kinyesi) wa rangi ya kijani au wenye mchanganyiko na damu au cheupe.
- Kukonda.
- Kukohoa.

Ukiona moja au zaidi ya dalili hizi katika kundi lako chukua hatua za kutibu zilizoelezwa hapa chini. Kama hali ni ngumu zaidi omba msaada kwa mtaalam wa tiba ya mifugo ili achunguze mara moja na kukushauri jambo la kufanya.

Muhtasari wa Magonjwa Muhimu ya Kuku na Jinsi ya Kuyadhibiti na Kutibu

Ugonjwa	Chanzo	Dalili	Kudhibiti na Kutibu
1. Kideri (Newcastle)	Virusi	Kukohoa, kupumua kwa shida. Mwili kukosa nguvu; shingo kujikunja. Kuharisha kijani. Kuku hufa wengi Kuhara damu.	Vifaranga wachanjwe katika juma lao la kwanza. Chanjo la pili wanapofikisha umri wa miezi 4 na nusu. Chanja kuku kila baada ya miezi mitatu.

Ugonjwa	Chanzo	Dalili	Kudhibiti na Kutibu
2. Kuhara damu (Coccidiosis)	Bakteria	Kuku hujikusanya pamoja. Hawachangamki. Hushusha mbawa.	• Tunza usafi katika banda. • Lisha vifaranga chakula kilichochanganywa na dawa ya kinga coccidiost kama Amprolium au Salfa. • Watenge kuku wote Walioambukizwa na wapatie dawa kama Amprolium au salfa au Esb3.
3. Ndui ya kuku (Fowl pox)	Virusi	Malengelenge kwenye kishungi na kope za macho na sehemu zisizo na manyoya.	• Kuchanja kuku wote wakiwa na umri wa miezi miwili. • Watenge kuku wote walioambukizwa na wapewe antibiotic kama OTC plus au salfa.
4. Mafua ya kuku (Fowl coryza)	Bakteria	Kuku uvimba uso na macho Kamasi hutirirka puani na mdomoni Kuhema kwa shida hata kukoroma. Kukohoa.	• Usafi wa banda • Kuchanja kuku wote • Kabla hawajaambukizwa kama ni tatizo sugu katika eneo • Watibu wanaougua kwa kutumia anti biotic kama sulphamethazine, streptomycine na vitamin
5. Kuharisha nyeupe	Bakteria	Kuharisha nyeupe na hamu ya kula kupungua. Wadudu washambuliao Kuku	• Usafi wa vyombo na banda kwa ujumla • Watenge kuku wagonjwa • Tumia dawa kama Furazolidone au Sulfadimidine • Hata vitunguu

			saumu menya robo kilo utwange nu kuchanganya na maji lita moja. Chuja uwapatie maji haya kwa muda wa wiki moja.
Wadudu washambuliao Kuku			
Viroboto,Chawa, Papasi		Kuku hawatulii, hujikuna mara kwa mara. Hupungukiwa na damu na uzito Wadudu huonekana mwilini	Wadudu washambuliao Kuku Usafi wa banda na mazingira Banda lipitishe hewa ya kutosha ili liwe kavu Nyunyizia kuku na banda zima dawa za kuua wadudu kama vile Akheri powder, Malathion, Servin n.k

Njia kuu za ujumla za kudhibiti magonjwa ni:

- Kutunza hali ya usafi ndani ya banda na kudhiditi kusiwe na unyevu
- Matandazo yakichafuka yabadilishwe.
- Vyombo vya maji visafishwe kila siku
- Jitahidi uepuke kufuga kwa njia ya huria ili kuku wako wasiambukizwe magonjwa kirahisi
- Epuka kufuga kuku wako pamoja na bata na khanga.Hawa ni wabebaji wa vimelea vya magonjwa ya kuku japo wao hubaki salama.
- Zingatia ratiba za chanjo kwa magonja yasiyo na tiba kama kideri na mengineyo ya virusi

Kutoa chanjo ya kideri kwa njia ya kuweka matone ya dawa katika macho

Kutoa chanjo ya kideri kwa njia ya kuweka matone ya dawa katika macho

Sehemu ya Sita

Kusimamia Ufugaji Wako

Kutunza kumbukumbu

Ili ufanikiwe katika ufugaji wa kuku, ni muhimu sana kulifahamu vyemi kundi la kuku wako. Ukilifahamu vema kundi lako utaweza:

Kuchagua kuku bora wa kuzalishia kwa kuangalia ubora wa wazazi wao.
Kufahamu historia ya afya ya kundi, kwa mfano

- Umri ambapo vifaranga vilipata chanjo.
- Ni chanjo ya aina gani.
- Magonjwa ambayo yamewahi kushuambulia kundi, na dawa ulizotumia katika matibabu.
- Idadi ya kuku wanaokufa.
- Kukadiria kiasi cha chakula ambacho kuku wako watahitaji kwa muda fulani na aina ya chakula.
- Kujua kila siku kuku wametaga mayai mangapi.
- Kujua utahitaji muda gani kutunza kuku toka vifaranga mpaka wanapofikia kuuzwa.

Ili uweze kufahamu mambo haya yote unahitaji kutunza kumbukumbu

Ufuatao hapa chini ni mfano rahisi wa kutunza kumbukumbu za kuku tangu wangali vifaranga mpaka wanapofikia uzito wa kuuzwa.

Mfano wa Kumbukumbu za ufugaji wa Kuku

Kumbukumbu ya Vyakula			
Tarehe	Kiasi cha Chakula (Kilo)	Kundi / Umri wa kuku na idadi yao	Maoni (Gharama, Kimetumika kwa muda gani nk)
	15	Vifaranga	
	25	Wanaokua	
Jumla			

Hapa utaweza kujua wastani wa matumizi ya chakula kwa idadi ya kuku na kwa kipindi husika.

Tarehe ya kuuza.....
Idadi iliyouzwa.....
Umri wa kuku wakati wa kuwauza.....
Mapato kutokana na kuuza.....

Kumbukumbu ya Kutibu Magonjwa			
Tarehe	**Magonjwa**	**Tiba**	**Maoni (vifo, gharama nk)**
3.7.2009	coccidiosis	teramycin	
5.9.2009	mdondo	furazolidone	

Kumbukumbu hii itakusaidia kujua magonjwa yanayosumbua mara kwa mara na kwa kipindi kipi. Pia na dawa inayosaidia zaidi kwa tatizo husika.

Chanjo au Kudhibiti magonjwa			
Tarehe	**Ugonjwa/Wadudu**	**Dawa**	**Gharama**
6.8.2009	Viroboto	Kunyunyiza doom powder au sevin powder	
5.10.2009	coccidiosis	Amprol katika maji, kinga dhidi ya	

Jinsi ya Kufahamu Faida Unayopata

Ili uweze kufahamu faida unayopata kutokana na ufugaji wa kuku inakupasa kutunza kumbukumbu za matumizi na mapato ya kila siku.

Kwa mfano:

Upande wa matumizi ingiza

- Gharama ya kununua vifaranga (kama walitotolewa hapo hapo nyumbani inafaa ukadirie gharama hiyo).
- Gharama ya chakula.

- Kama unatengeneza na kuchanganya wewe mwenyewe kadiria kwa kutumia bei za viungo ghafi.
- Gharama ya mafuta ya taa (kama uliwakuza vifaranga kwa joto la taa).
- Gharama ya kusafisha banda kubadili matandazo.
- Gharama za madawa ya kinga (chanjo) na tiba.

Upande wa mapato ingiza mapato kutokana na:

- Mauzo ya mayai.
- Mauzo ya kuku hai.
- Gharama ya mayai yaliyotumiwa nyumbani.
- Mauzo ya mbolea kutoka katika banda.

Ufuatao ni mfano unaoonyesha jinsi ya kuingiza taarifa hizi katika daftari la kumbukumbu .

Kumbukumbu ya Kutibu Magonjwa					
Tarehe	**Matumizi**	**Sh.**	**Tarehe**	**Mapato**	**Sh.**
	Kununua vifaranga 30 @ 200/=	6,000/=		Mauzo ya mayai 10 @150/=	1,500/=
	Kununua vyakula kilo 10 @150/=	1,500/=		Mayai na kuku waliotumiwa nyumbani	7,000/=
	Dawa ya kukohoa 1500/=	1,500/=		Mauzo ya kuku 20 @ 4000/=	80,000/
	Dawa ya wadudu 1000/=	1000/=		Mbolea iliyouzwa	
	.....nk.	..... nk		.... nk	
Jumla					

Baada ya kufanya mauzo yote ya kundi jumlisha matumizi yote na jumlisha na mapato yote katika kipindi kizima cha kufuga.

Ili kufahamu faida uliyopata fanya hesabu hii:

Jumla ya Mapato yote - Jumla ya Matumizi yote = Faida

Sehemu ya Saba

Masoko

Katika biashara ya aina yoyote mzalishaji hana budi afahamu mambo kadhaa ya msingi yatakayomsaidia kufanya maamuzi ya kumuwezesha kupata faida ya juu katika biashara anayoifanya:

Kwanza kabisa ajiulize kama bidhaa anayozalisha ina soko? Na kama soko lipo:

- Lipo wapi na hali ya miundombinu za kulifikia iko vipi (ili afahamu gharama ya kufika sokoni kama utaamua kuuzia sokoni).
- Bidhaa inahitajika kwa wingi kiasi gani na wakati gani sokoni
- Soko linahitaji bidhaa yenye sifa zipi (ubora n.k. ili uzalishe sawa na matakwa ya soko n.k)
- Kama wanunuzi watakuwa na utayari kununulia unakozalishia, je unao uwezo wa kutosheleza mahitaji yao (ili uweze kujipanga kukidhi mahitaji kwa kuongeza uzalishaji au kwa kuungana na wazalishaji wengine).
- Linganisha bei ya bidhaa sokoni na bei ya kuuzia unakozalishia (ili ujue palipo na faida zaidi kwako baada ya kuondoa gharama za kufuata soko) Ila ukiamua kuuzia sokoni hakikisha unao uwezo wa kushindana na wauzaji wengine huko sokoni.

Majibu ya maswali haya ndiyo yatakayokupa msingi wa kujipanga kiuzalishaji ili hatimaye upate faida. Hivyo hata kabla hujaanza kuzalisha fahamu haya yaliyotajwa hapa juu.
Kutafuta na kutumia taarifa za masoko ya sehemu tofauti

Kwa kadri utakavyokuwa unaendelea kuzalisha, mabadiliko mbali mbali yatatokea kuhusiana na uzalishaji wako na hata kuhusiana na soko la bidhaa unayozalisha kwa maana ya kuku.

Ili uendane na mabadiliko yanayotokea ni muhimu mzalishaji upate taarifa za hali ya soko mara kwa mara. Taarifa hizi zitakusaidia kufanya maamuzi yatakayokuwezesha kuendelea kupata faida.

Taarifa za masoko zinaweza kupatikna kwa wazalishaji kadhaa kuungana na kuunda umoja wao. Katika umoja huo wawakilishi wachache wanakuwa na jukumu la kutafuta taarifa za masoko ya kuku sehemu mbali mbali ambako kunaweza kuwapa wazalishaji tija zaidi.

Walio katika umoja huo watatumia taarifa hizo kufanya maamuzi ya kuuza kwa faida zaidi kwa pamoja au kwa mmojammoja kutegemeana na hali halisi. Watoa taarifa pia

watafanya mawasiliano ya kuwajulisha wanunuzi juu ya upatikanaji wa kuku kwenye maeneo wanakozalishiwa.

Mbinu zaidi ya kupata masoko mazuri

Umoja wa kuzalisha na kuuza

Kwa kawaida kama bidhaa ina soko, wateja hupatikana kwa urahisi pale wanapohakikishiwa upatikanaji wa bidhaa kwa wingi katika sehemu moja.

Katika hali hii, wanunuzi huwa tayari hata kununua kwa bei ya juu zaidi kwa sababu ya kupunguza muda na gharama ya kutafuta bidhaa ya kutosha kupeleka sokoni.

Kwa upande wa kuku jambo hili linawezekana kama mfugaji atafuga kuku wengi wa umri usiopishana sana kwa wakati mmoja. Watakapofikia kimo kinachofaa kuuza utawauza wengi kwa wakati mmoja na kwa faida zaidi.

Mahali ambapo mfugaji mmoja mmoja hawezi kukidhi wingi wa hitaji la wanunuzi, wafugaji kadhaa wanaweza kuunda umoja wao wa kuzalisha (kila mmoja kwake) na kuuza kwa kipindi kimoja na kupata faida zilizotajwa hapa juu.

Faida nyingine ya kuuza katika umoja ni kuongezeka kwa uwezo wenu wa kupanga na kusimamia bei mnayotaka kuuzia. Sauti na uamuzi wenu wa pamoja utawapa nguvu ya kusimamia bei yenu mnayoipanga dhidi ya bei za chini wanazotaka wanunuzi. Uwezo wako wa kusimamia bei unyoitaka ni mdogo ukiuza peke yako.

Sehemu ya Nane

Chama cha Akiba na Kukopa

Chama cha akiba na mikopo ni kikundi cha watu waliojiunga kwa hari yao kufanya ushirika wa kuweka akiba zao kwa pamoja na kutoa mikopo kwa urahisi kutokana na akiba zao.

Kwa wafugaji wa kuku kubiashara wanashauriwa kuwa na chombo cha namna hii kitakachokuwa na utaratibu wa wanachama kuweka na pia wanachama hawa kuwa na fursa ya kukopa kwa lengo kubwa la kuendeleza ufugaji wao kuku kibiashara.Ufugaji wa kibiashara ungehitaji kuongeza mtaji mara kwa mara kulingana na mahitaji ya soko husika. Mfumo wa kuweka na kukopa utakuwa chanzo kizuri na cha kuaminika kukidhi haja ya mtaji endelevu kwa wafugaji wa kuku.

Michango kwa ajili ya akiba inaweza kutokana na makato ya mapato yanayotokana na mauzo ya bidhaa za kuku (vifaranga,mayai, kuku n.k.). Au kiwango maalum kwa wakati maalum kinaweza kuwekwa na wanachama ili kitolewe kwa utaratibi wanaokubalianana. Wanachama wanaweza kukopa kutoka kwenye chama chao kwa ajili ya ununuzi wa mahitaji,mbalimbali ya kuku kama:

- Madawa
- Vyakula
- Ukarabati au ujenzi wa mabanda ya kuku n.k

Faida za chama kama hiki ni:

- Wanachama watapata sehemu ya kuhifadhi pesa yao kwa usalama kwa ajili ya matumizi ya baadaye.
- Masharti ya kukopa ni nafuu kuliko vyombo vingine vya kifedha.
- Wanachama hujifunza misingi ya kushirikiana, mahusiano na kusaidiana.
- Wanachama hupata maarifa ya ziada kuhusu maswala ya kifedha.

Chama cha namna hii, lazima kiwe na kanuni za kukiongoza ambazo hutungwa na wanachama wenyewe.

Kanuni hizi zilenge kulinda malengo ya chama na kila mwanachama anawajibika kuzizingatia.

Mambo makuu ya kuzingatia katika katiba ni:

- Malengo ya chama
- Haki, wajibu na malengo ya wanachama
- Viwango vya viingilio
- Hisa na michango
- Uongozi na majukumu
- Vikao na mikutano
- Utunzaji wa kumbukumbu
- Mikopo na riba
- Taratibu za kutoa mikopo
- Migawanyo ya faida

Mambo ya msingi ya kusimamia na kuendesha chama cha Akiba na Kukopa ni pamoja na:

- Uhiari wa wanachama
- Uongozi uwe wa kidemokrasia
- Kusiwe na urasimu
- Chama lazima kiwe na vitabu vitakavyotumika kuweka kumbukumbu ya hifadhi za fedha za wanachama
- Uwekaji wa akiba uwe wa mara kwa mara
- Mkopo ulipwe kwa muda uliopangwa
- Fedha za chama ziwekwe benki au kwenye masanduku maalum ya kutunzia kwa utaratibu uliopendekezwa Mahesabu ya chama yafanyiwe ukaguzi mara kwa mara.

Kikundi kama hiki kinaunganisha nguvu pamoja na kupunguza tatizo la kupata huduma ya kifedha hasa katika maeneo ya vijijini.Hata hivyo jambo la msingi la kufanikisha malengo ya vyombo hivi ni kuzingatia kanuni zilizowekwa na wahusika. Vilevile utaalam wa kutosha wa kuendesha na kusimamia chombo vya namna hii ni muhimu uwepo.

RURAL LIVELIHOOD
DEVELOPMENT COMPANY

Jengo la NBC
Ghorofa ya Pili, Mtaa wa Nyerere
S.L.P. 2978, Dodoma, Tanzania.
Simu +255 26 2321455, Faksi +255 26 2321457.
Barua pepe: info@rldc.co.tz.
Tovuti: www.rldc.co.tz.